

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe: press@ikulu.go.tz
Tovuti: www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Singida
15 Oktoba, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RAIS SAMIA AANZA ZIARA YA KIKAZI MKOANI SINGIDA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema serikali itaendelea kuhakikisha huduma ya elimu inasogezwa karibu na wananachi ili kuondoa adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

Rais Samia amesema hayo leo wakati akihutubia wananchi katika eneo la uwanja wa Police Square wilayani Manyoni ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya kikazi mkoani Singida.

Rais Samia amesema kupitia mradi wa Kuimarisha Elimu ya Awali na Msingi nchini (BOOST) na Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) serikali inajenga shule za msingi na sekondari katika mikoa yote nchini.

Rais Samia amesema lengo la miradi hiyo ni kuondoa msongamano katika madarasa ili kuongeza tija na ufanisi kwenye ufundishaji kutoka wanafunzi 120 kwa darasa hadi kufikia 45.

Awali Rais Samia alifungua Shule ya Msingi Imbele yenye thamani ya shilingi milioni 493.4 na mabweni ya madarasa ya Shule ya Sekondari Mwanamwema Shein katika Manispaa ya Singida.

Rais Samia pia aliweka Jiwe la Msingi, ujenzi wa barabara ya Mkiwa - Itigi - Noranga (56.9km) kwa kiwango cha lami yenye thamani ya shilingi bilioni 67.2 bilioni ambayo ni sehemu ya barabara ya Makongorosi- Rungwa - Itigi - Mkiwa (413km).

Barabara hii licha ya kuunganisha ushoroba wa Tanzania na Zambia pamoja na wa kati itaunganisha pia Tanzania na ukanda wa SADC na hivyo kuchochea shughuli za uzalishaji na biashara kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

